

# KUSHINDA MITHALI ZA NCHI

James Kalekwa

# KUSHINDANA NA MITHALI ZA NCHI.

James Kalekwa

# Orodha ya Yaliyomo

USICHOKUJUA KUHUSU MITHALI .................................. 4

MITHALI ZA NCHI NI NINI? ............................................... 9

MITHALI ZA NCHI AU NENO LA MUNGU?.................. 14

KUNA MITHALI NJEMA PIA ....................................... 17

MIFANO YA KUPINDUA MITHALI ZA NCHI ............... 19

Mfano wa Manase na Efraimu (Mwanzo 48:8-20)........... 19

YAKOBO SHUJAA WA IMANI..................................... 23

Kuhusu Mwandishi:.............................................................. 25

Kuhusu New Vine Church:.................................................... 25

Mawasiliano na Mwandishi: ................................................. 26

# USICHOKUJUA KUHUSU MITHALI

Kuna mithali halafu kuna yaliyositirika nyuma ya mithali. Kwenye surah ii ya kwanza nimekusudia, kwa njia ya neno la Mungu, kuchana pazia linaloficha. Baada ya kusoma surah ii hautaishia kujua uwepo wa mithali fulani bali kujua yaliyo nyuma ya mithali. Roho Mtakatifu akufumbue macho uone sawasawa!

*"22. Mwanadamu,* ***ni mithali gani hii mliyo nayo katika nchi ya Israeli****, mkisema, Siku hizo zinakawia na maono yote hayatimizwi. 23. Basi uwaambie, Bwana MUNGU asema hivi;* ***Nitaikomesha mithali hii, wasiitumie tena kama mithali katika Israeli****; lakini uwaambie, Siku hizo ni karibu, na utimilizo wa maono yote."* **Ezekiel 12:22-23**

*"Je! Maana yake ni nini hata* ***mkatumia mithali hii katika Israeli,*** *mkisema, Baba wamekula zabibu mbichi, nao watoto wakatiwa ganzi la meno? 3. Kama mimi niishivyo, asema Bwana MUNGU,* ***hamtakuwa na sababu ya kuitumia tena mithali hii katika Israeli.****"* **Ezekieli 18:2-3**

*“Tazama, **kila mtu atumiaye mithali atatumia mithali hii kinyume chako**, akisema, Kama mama ya mtu alivyo, ndivyo alivyo binti yake.”* **Ezekieli 16:44**

Kutokea kwenye maandiko yaliyorejelewa hapo juu, kuna mambo kadhaa yasiyojulikana kwa uwazi kuhusu mithali. Ningetamani sana kwa kusoma kitabu hiki yakufunukie kwa haraka na upesi. Ninakuombea ya kwamba Roho Mtakatifu atavuviwa ufahamu wako haraka ili yasiwe kificho mbele zako, katika jina la Yesu Kristo!

Mosi, **mithali huwa ni kwa ajili ya watu wa eneo fulani tu.** Taifa la Israeli lilikuwa na aina fulani ya mithali ambazo zilikuwa zinatumika kwao tu. Hii kutokana na uzoefu wa zama zao ya kwamba Mungu akiahidi inachukua muda fulani kutokea na inawezekana hata waliosikia hiyo ahadi wasiione ikitokea. Wakaamu kutunga mithali kuulezea uzoefu wao kumuhusu Mungu. Hata hivyo, hiyo ni mithali inayotumika katika Israeli tu – usisahau hilo! Kuna mithali ni za eneo fulani, jamii, zama, kizazi au nchi tu wala sio za dunia nzima. Kuna mithali za Israel tu.

Pili, **mithali huanzishwa na hufutwa**. Moja ya mambo yaliyowahi kunishangaza ni ugunduzi huu. Siku nilipotambua ya kwamba mithali huwa zina muda wake wa kuishi- huwa zinaanzishwa na pia inawezekana kuzifuta kabisa. Mungu anasema na watu wan chi ya Israeli ya kwamba *"hamtakuwa na sababu ya kuitumia tena mithali hii katika Israeli."* Inanipa kuona ya kwamba kumbo zinaweza kufikia ukomo. Au asemapo, "*Nitaikomesha mithali hii, wasiitumie tena kama mithali katika Israeli…"* ninapata utambuzi ya kwamba mithali zinaweza kuwekewa ukomo wa matumizi kwenye eneo. Hakuna mithali ya milele! Hakuna mithali ya muda wote!

Tatu, **mithali hutumika kwa sababu fulani kwenye eneo**. Zinatumikia na kutimiliza kusudi fulani. Pale ambapo anaeleza ya kwamba hawatakuwa na sababu tena (Ezekieli 18:3). Ooh! Kumbe mithali zipo kwa sababu fulani. Mithali zinaelezea uzoefu, historia, utamaduni au mwenendo wa watu au jamii ya eneo fulani kuhusiana na jambo fulani. Sababu ya uwepo wa mithali ikiisha, basi na mithali imeisha. Vilevile, kama

mithali haielezei uzoefu au mwenendo wako kuhusiana na jambo hilo, huna sababu ya kuitumia mithali hiyo.

Nne, **mithali zinaweza kutumika kinyume cha maisha ya mtu au watu**. Angalia kile ambacho Mungu anakisema kuhusiana na watu wanaotumia mithali. Kumbe wanaweza kuitumia kinyume na maisha ya mtu (Ezekieli 16:44). Inawezekana kusudio la awali la utunzi wa mithali hiyo lilikuwa jema kabisa; inawezekana mithali hiyo imekuwa ikitumika kwa uchanya muda wote. Halafu ghafla, watu fulani, ili kutimiliza matakwa yao, wanaanza kuitumia mithali hiyo kinyume chako na maisha yako kwa ujumla wake.

Tano, **mithali huwazuilia watu wasiende mbele kimaisha kama Mungu alivyokusudia**. Moja ya adui mkubwa wa mwanadamu hata si shetani bali ni mithali zilizomo kwenye nchi. Kama nilivyokuonyesha hapo juu ya kwamba mithali zinaweza kutumika kinyume chako na mambo yanahusiana na wewe; vilevile, mithali zinakuminya usione utimilifu wa ahadi za Mungu kwenye maisha yako nay ale yanayohusiana na wewe.

Kilichokuwa kinawazuilia wana wa Israeli siyo pepo wala shetani ila ni mithali!

Sita, **Mungu hupambana na mithali za nchi ili atupeleke kwenye kiwango alichokusudia kwenye kila eneo la maisha**. Kwenye maandiko yaliyorejelewa hapo juu utagundua ili Mungu aachilie upako wa kutanuka kwenye maisha ya mtu au watu, moja ya vitu ambavyo atapambana navyo ni mithali, na hiyo mithali ni ya eneo fulani tu… mithali ya nchi!

Mungu anataka tufanikiwe na kutanuka lakini kinachopingana na sisi ili kutuzuia ni mithali za nchi; Mungu anataka atupe afya lakini kinachotuzuia ni mithali *"Wanadamu tumeumbiwa maradhi"*.

Kuna mithali inayozuia watu wasijiendeleze kielimu na ufahamu *"kiingereza kimekuja na meli"* hii inazuia watu kujifunza.

Kuna mithali ambazo zinawawekea watu ukomo *"shida tumeumbiwa wanadamu"*; *"hujafa ujaumbika"* hizi ni mithali za nchi ambazo zinazuia usione msaada wa Mungu.

# MITHALI ZA NCHI NI NINI?

Baada ya kufanya ugunduzi wa yaliyositirika kwa muda mrefu kuhusiana na mithali. Sasa, tunaoujasiri ya kwamba hakuna kilichositirika kwetu kuhusiana na mithali. Ninaamini utaanza kuwa makini kwenye masikio, kinywa na midomo yako kuhusiana na mithali.

- Mithali ni maneno, misemo na tungo ambazo huchukuliwa kama kweli na watu wa eneo husika. Mara zote hizi tungo na misemo watu wa eneo fulani huwa wanajitengenezea, kwa hiyo ukitaka kuishi katika eneo hilo haupaswi kuenenda kinyume na hizo

mithali. Mfano ni ngumu kusema *“nina afya au mimi ni mzima.”*, watakuzuia kwa kukwambia wewe *“hujafa, hujaumbika”;* ni ngumu sana kusema Bwana amenibariki najenga nyumba nzuri maana itaonekana unajivuna ,unapaswa sema *“tunajenga kakibanda”….* Unafikiri ni unyenyekevu kujenga kibanda?

*“Nao watajenga nyumba, na kukaa mdani yake…”* Isaya 65:21

Kibiblia, vibanda vilitumika kwa ajili ya makazi ya muda nje ya makazi ya kudumu. Na ilikuwa ni kwa ajili ya sikukuu mahususi kwa Wayahudi; Sikukuu ya vibanda, *“Mtakaa katika vibanda muda wa siku saba; wazalia wote wa Israeli watakaa katika vibanda.”* **Mambo ya Walawi 23:42 (SUV)** Soma kwa kulinganisha na andiko hili, *“Ni sikukuu ya Wayahudi, Sikukuu ya Vibanda, ilikuwa karibu.”* **Yohana 7:2 (SUV)**;

*“Musa, akawaamuru, akasema, Mwisho wa kila mwaka wa saba, wakati wa maachilio, wakati ulioamriwa wa*

*sikukuu ya vibanda.”* **Kumbukumbu la Torati 31:10 (SUV)**

Hata hivyo matumizi ya msingi kabisa ya vibanda yalikuwa ni kwa ajili ya mifugo iliyopo kwenye makazi ya watu; au kwa ajili ya mifugo na wachungaji wake iwapo mifugo ipo nje ya makazi ya watu.

*“Yakobo akaendelea mpaka Sukothi. Akajijengea nyumba, akawafanyia makundi yake vibanda. Kwa hiyo jina la mahali pale kaitwa Sukothi.”* **Mwanzo 33:17 (SUV)**

*“Na hiyo nchi ya pwani itakuwa malisho, yenye vibanda vya wachungaji, na mazizi ya makundi ya kondoo.”* **Sefania 2:6 (SUV)**

Hapa nimewekeza muda mwingi kujenga hoja kwa ushahidi mwingi wa kimaandiko kukunyesha walau mfano huu mmoja. Unafikiri ni unyenyekevu kusema unajenga kibanda wakati unajenga nyumba? Unafikiri ni sawa kuinena hivyo baraka ya Bwana? Kama Mungu amekubarikia na unajenga nyumba…. Mpenzi, iseme baraka ya Bwana kwa lugha ambayo Mungu anaisema!

- Ni tungo zinazoendana na mazingira na muktadha wa mahala husika (contextual and subjective). Sasa ili miji iendelee inahitaji watu wasio wa hiyo miji wasio amini mithali za mahala hapo waje na kuzikanusha ndipo mji au eneo litafumuka; au watu wazawa wa eneo hilo watoke na kwenda mbali na mazingira yao kisha warudi wakiwa huru kwenye fahamu zao ili wabomoe mithali hizo; au Mungu avuvie mzawa na apokee ufahamu kinyume na mithali zilizowashikilia kwa muda mrefu. Na njia bora kuliko zote ni watu, wazawa ama wageni, wasikie kweli ya neno la Mungu kuhusiana na jambo fulani. Kisha waishikilie kweli hiyo ambayo mara zote itaenda kinyume na mithali za nchi. Hapo ndipo kuna mpenyo utatokea!

- Mithali huelezea ufahamu wa kiuzoefu wa kundi la watu wa mahala fulani (experiential knowledge). Hawa watu ukiwakalisha sehemu ambayo uzoefu wa kwenye jamii yao hayapo wasingekua na hizo mithali.

- Mithali huwawekea watu mipaka na ukomo katika eneo husika au huwahamasisha kua wakuu zaidi. Lakini kuna mithali inakuzuilia kabisa kuwaza mafanikio *"ng'ombe wa masikini hazai na akizaa huazaa dume",* hii mithali inakuzuia usiwe na bidii.

- Mithali hutungwa na mtu yeyote na kuzisambaza, kuna methali unapaswa kua makini nazo kwa nje zinaonekana kama hekima lakini ndani zina mtego.

- Watu wema na waovu wote hutunga mithali; Sasa inategemea hiyo mithali unayoitumia ametunga nani. Kwa mfano kuna nyimbo wameimba wapumbavu, yaani wawasilishaji wa nyimbo hizo (fanani) ni wapumbavu; na kuna nyimbo zimetungwa kwa ajili ya (wameimbiwa) wapumbavu tu – yaani, hadhira iliyokusudiwa ni ya wapumbavu; na kuna nyimbo ambazo maudhui yake ndiyo upumbavu wenyewe, yaani kilichomo ndani ya wimbo.

*"Heri kusikia laumu ya wenye hekima, Kuliko mtu kusikia wimbo wa wapumbavu."* **Mhubiri 7:5 (SUV)**

Huwa ninapenda kuwashauri, hususani vijana, usiingilie nyimbo ambazo hazikuhusu kiasili. Ukiendelea kusikiliza nyimbo ambazo haukukusudiwa tangu awali uzisikilize, muda si mrefu utakuwa kama waliokusudiwa. Sasa, ndivyo ilivyo kwa mithali… kuna mithali haukukusudiwa kuzitumia.

# MITHALI ZA NCHI AU NENO LA MUNGU?

Tumefika mahala pa kuchagua njia ya kuiendea… baada ya sura mbili zilizotangulia. Hupaswi kubakia njiapanda. Sasa, kabla haujafanya maamuzi ya mwisho. Uniruhusu nikutazamishe upande mmoja kuhusu neno kisha uwe huru kuchagua vyema.

*"Mbingu na nchi zitapita; lakini maneno yangu hayapita kamwe."* **Mathayo 24:35**

Mithali si kweli, ila neno la kristo ndiyo kweli. Ndiyo, mithali zinaweza kusema uhalisia (facts) lakini hazina kigezo cha kweli (truth). Ni vyema ulewe ya kwamba kweli huwa ni moja. Kama kunaweza kuwa na kweli nyingi kuhusiana na jambo moja basi zote zinapoteza vigezo vya kuwa kweli. Sasa, neno la Mungu:

- ✓ Ni kweli ya milele (eternal truth)
- ✓ Ni kweli popote (universal truth)
- ✓ Ni kweli isiyoegamia upande wowote (objective truth)
- ✓ Ni kweli yenye mamlaka ya mwisho (absolute truth)

Neno la Mungu ni ni mamlaka ya mwisho (final and conclusive) kwenye maisha. Halina mbadala wala halina mjadala!

Upande wa pili ni kwamba, mithali huwa zinapitwa na wakati; mithali siyo jambo la ulimwengu wote (universal). Zingatia ya kwamba kama Neno lilileta matokeo Israel litaleta matokeo katika eneo lako au mtaa

wako pia. Kama neno lilileta matokeo kwa Musa litaleta matokeo kwako; neno huwa halibagui watu.

- Mithali ni matokeo ya utamaduni, mila desturi na mapokeo ya kundi fulani la watu.
- Mithali zinaweza kuwa za hila, uongo na udanganyifu kuna vitu ni misemo lakini ni hatari kwenye ufahamu wa mwanadamu (Ezekiel 11:1-2). Hutungwa kutokea shimo la kuzimu na kuachiliwa kwenye mji ili kupotosha watu.

Usiende na dunia inavyoenda unapaswa kusimika mizizi yako kwenye neno.

Ili uweze kufanikiwa na kutanuka katika eneo lako lazima ujifunze kupingana na mithali za nchi kama vile…

- "tumeumbiwa maradhi"
- "tafuta hela"
- "Kingereza kimekuja na meli"
- "hakuna upendo wa kweli"
- "wanaume wote baba yao ni mmoja"
- "vijana ni taifa la kesho"

Orodha ya Mithali za nchi za kupingana nazo ni ndefu…

Soma kwenye KITABU kuna hekima nyingi, acha kujifariji na mithali za wajinga chukua hatua ya kujifunza na kufanyia kazi mambo yote yaliyo mema!

## KUNA MITHALI NJEMA PIA

Habari njema ni kwamba kuna Mithali njema nyingi tu ambazo zinaweza kuyaongoza maisha yako! Hizo shikamana nazo, ambatana nazo.

Hizi ni Mithali ambazo ni matokeo ya mafundisho mema kweli zinazopaswa kukumbatiwa. Hebu tazama andiko hili kisha turudi kuhitimisha.

*"Walakini, kwa sababu huyo Mhubiri alikuwa na hekima, aliendelea kuwafundisha watu maarifa, naama, akatafakari, akatafuta-tafuta, akatunga mithali nyingi."* **Muhubiri 12:9 (SUV)**

Baadhi ya mithali hizi ndizo zinaunda kile kitabu cha Mithali cha kwenye Biblia.

Ukimaliza kupingana na mithali za nchi, ninaweka changamoto mbele yako uingie kwenye jukumu la kutunga mithali ili ziweae kutumiwa na watu.ala ya kumucha shetani na kambi yake kuchukua nafasi ya heshima kwenye kutengeneza mithali zinazotumika dunia na kwenye maeneo mbalimbali… ni muda wako kama mwamini kua jopo wa watunga mithali wa nchi.

Ndugu mmoja aliwahi kufundisha na kusema, ukitaka kuibadilisha nchi wala usijidanganye kubadilisha katiba! Jinsi ya kuigeuza nchi kabisa, hakikisha unapenyeza ajenda za mabadiliko kwenye kazi ya fasihi ya taifa husika… kwa mfano, ukitunga misemo na maneno yatakayotumika kitaifa! Na muda si mrefu badiliko la mithali litazaa badiliko la kimtazamo miongoni mwa watu. Kisha watu wao wenyewe watafanya jukumu la kuibadilisha katiba na mifumo inayoongoza na kuratibu nchi. Na jambo hilo litatokea bila kuhitaji ruhusa ya mtu yeyote wala kukusanya maoni popote. Litakuwa ni jambo halali na lenye kukubalika mbele ya wote.

Chagua kulilisha taifa kwa mithali mpya za nchi zilizojaa uungu ndani yake.Je, utafanya hivyo?

# MIFANO YA KUPINDUA MITHALI ZA NCHI

Si unamjua adui mkubwa wa mithali za nchi ni nani? Ni Mungu mwenyewe! Kwenye sura hii tutatazama Mungu akifanya "ukatili" dhidi ya mithali za nchi kwa uvuvio aliouweka ndani ya watu wake.

## MFANO WA MANASE NA EFRAIMU (MWANZO 48:8-20)

Ili uweze kuelewa kile utakachojifunza kwenye surah ii, ni vyema ukachukua Biblia yako kisha ukasoma kifungu chote nilichotangulia kukiainisha hapo juu. Hiyo itakujengea kuelewa kwa upana mazingira ya andiko. Hapa nitanukuu baadhi tu ya mistari.

*"13. Yusufu akawaweka wote wawili, Efraimu katika mkono wake wa kuume, kuuelekea mkono wa kushoto wa Israeli (Yakobo); na Manase katika mkono wake wa kushoto, kuuelekea mkono wa kuume wa Israeli, akawasogeza karibu. 14. Israeli akanyosha mkono wake wa kuume akauweka juu ya kichwa cha Efraimu,*

*aliyekuwa mdogo, na mkono wake wa kushoto akauweka juu ya Manase, huku akijua atiavyo mikono; maana Manase ndiye aliyezaliwa kwanza. 17. Naye Yusufu alipoona kwamba babaye anaweka mkono wake wa kuume juu ya kichwa cha Efraimu, ikawa vibaya machoni pake. Akauinua mkono wa babaye auondoe katika kichwa cha Efraimu, ili auweke juu ya kichwa cha Manase. 18. Yusufu akamwambia babaye, Sivyo, babangu, maana huyu ni mzaliwa wa kwanza; weka mkono wako wa kuume kichwani pake. 19. Babaye akakataa, akasema, Najua, mwanangu najua, yeye naye atakuwa taifa, yeye naye atakuwa mkuu; lakini ndugu yake mdogo atakuwa mkubwa kuliko yeye, na uzao wake watakuwa wingi wa mataifa."* **Mwanzo 48:13-19**

Huu ni ule mtiririko wa kimuundo wa baraka kutoka kizazi kimoja kwenda kingine; ni utaratibu ya kuwa mzaliwa wa kwanza ndiye alipewa kupokea urithi mara dufu (double portion).

Yusufu aliwapeleka wanawe Manase na Efraimu kwa Yakobo awabariki; na akawapanga kulingana na mithali ya nchi au utaratibu kwamba wa kwanza akae kulia na

wa pili kushoto. Lakini mzee Yakobo akachanganya mikono hali akijua anachokifanya.

Hebu tazama matokeo yam zee Yakobo kuchanganya mikono kinyume na mithali au utaratibu uliozoeleka. Si unajua makabila kumi na mbili ya taifa la Israeli, kimsingi, ni majina ya wana kumi na mbili wa Mzee Yakobo? (Soma Mwanzo 49:1-); Ninakusihi uyasoma majina haya bila kuruka… sijayaorodhesha hapa kama mapambo: Reubeni, Simeoni, Lawi, Yuda, Zabuloni, Isakari, Dani, Gadi, Asheri, Naftali, Yusufu na Benyamini.

Sasa, kwa ufahamu huo, hebu soma maandiko kadhaa ninayoambatanisha hapa:

*"Tena Yoshua akawaambia Wareubeni, Wagadi, na hao wa nusu* ***ya kabila ya Manase****."* **Yoshua 1:12 (SUV)**

*"Wa kabila ya Asheri kumi na mbili elfu. Wa kabila ya Naftali kumi na mbili elfu.* ***Wa kabila ya Manase*** *kumi na mbili elfu."* **Ufunuo wa Yohana 7:6 (SUV)**

Zingatia hili ya kwamba kwenye orodha ya wana kumi na mbili ambao ndiyo makabila ya Israeli kiasilia,

Manase hayumo. Kiutaratibu, Manase ni mjukuu wa Israeli. Kwa misingi hiyo, hawezi kusomeka kwenye orodha moja pamoja na baba zake. Hawezi kuwa kwenye ligi ya wazee wake! Hakuwa na vigezo vyovyote vile vya kusomeka kwenye ligi iliyo juu yake… yeye ni mjukuu na pia ni mzaliwa wa pili. Kimsingi, hakuna hata sababu moja ambayo inaweza kutumika kama hoja ya kumpa uhalali Manase kusoma kwenye ligi ya baba zake.

Hicho ndicho ambacho hutokea pale Mungu anapoingilia kati; anachanganya mikono na kuvunja taratibu na mithali zinazoongoza maisha ya watu!

Inawezekana kwa ukoo wako, kabila, elimu au sababu yeyote unaweza kujiona huwezi mambo fulani kutokana na mithali za eneo husika lakini Mungu anaweza badilisha mambo… anaweza KUCHANGANYA MIKONO!

Mikono ikichanganywa unapandishwa hadhi, yale ambayo hayakuWa ya kawaida yatatokea kwako kwa ukawaida sana kwa kuwa Bwana atavunja utaratibu

# YAKOBO SHUJAA WA IMANI

Mzee Yakobo anasomeka kwenye orodha ya mashujaa wa Imani wa kitabu cha Waebrania 11. Uzuri neno la Mungu liko wazi sana. Linaonyesha kila shujaa wa Imani na sababu iliyompelekea kuingia kwenye orodha hiyo.

Ninatambua fika ya kwamba tunaweza kukubaliana ya kwamba Yakobo alikuwa na nyakati za ajabu za upekee na Bwana kwenye maisha yake. Baadhi ya nyakati hizo ni kama vile:

a) Kupumzisha kichwa chake kweye lango la mbinguni na ile ndoto ya malaika kupanda na kushuka (Mwanzo 28:12-17)
b) Kuzidishiwa mali na umiliki wake (Mwanzo 31:10-13)
c) Kupigana mieleka na malaika na kujipatia mgeuko mkubwa wa maisha yake (Mwanzo 32:22-32)
d) Kubadilishwa jina na kuwa na jina ambalo taifa linaitiwa ulimwenguni (Mwanzo 35:9-15)

Pamoja na nyakati hizo za kusisimua, nzuri na zilizojaa mguso mkubwa. Hata hivyo, hakuna hata moja kati ya hizo iliyomuingiza kwenye jumba kubwa la mashujaa wa Imani.

Jambo pekee ambalo linaonekana ni jambo la kiimani ni hili:

*"Kwa imani Yakobo, alipokuwa katika kufa, akambariki kila mmoja wa wana wa Yusufu, akaabudu akiegama kichwa cha fimbo yake."* **Weaebrania 11:21 (SUV)**

Hakuna tena maelezo mengine ya kwanini ameonekana kwenye kitabu hiki cha mashujaa wa imani. Ninajua unaelewa namna aliyoitumia kuwabariki Efraimu na Manase! Aliwabariki kwa "kuvunja mithali" ya wakati huo. Na hilo lilisomeaka kama tendo la imani. Hii imani ni lazima itakuwa imevuviwa na kuchochewa na utendaji wa kiungu ndani yake. Si kawaida mwanadamu kuwaza juu namna hii.

Ninakuombea, Mungu avuvie ndani yako aina ya imani ambayo itakupeleka juu ya mithali zinazokuzuilia usipige hatua.

## Kuhusu Mwandishi:

Mwandishi wa kitabu hiki, James Kalekwa, ni mfuasi wa Yesu Kristo; mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; Mume mpenzi wa Frida, baba anayewajibika wa Joshua-Vision, Charis “Tai”, Victor na Priscilla; na anafurahia kuwa mchungaji mkazi wa kanisa la New Vine jijini Dodoma.

Mchungaji James ameitwa *“Kuujaza ulimwengu kwa maarifa ya utukufu wa Mungu kama maji yaifunikavyo bahari.”* [Habakuki 2:14]

## Kuhusu New Vine Church:

Kanisa la New Vine limebeba utume wa kuinua kizazi cha kiungu kitakacholeta mguso chanya kwenye kila nyanja ya maisha kwenye jamii, taifa na mataifa. (Mathayo 5:13-14/Yoeli 2:2-11)

Makao makuu ya kanisa (Gloryland) yako Mwanza chini ya mwangalizi ambaye pia ni muasisi, Mchungaji Goodluck & Mama Ziada Kyara.

Kufahamu zaidi kuhusu kanisa hili kwa ujumla tembelea: https://www.newvinechurch.or.tz

## Mawasiliano na Mwandishi:

Iwapo unahitaji kupata mafundisho zaidi ya maandishi na audios kutoka kwa mwandishi wa Kitabu hiki, Mchungaji James Kalekwa. Unaweza kufanya hivyo kupitia channel ya telegram: https://t.me/nvcdodoma AU fungua app ya telegram kisha tafuta @nvcdodoma

Unaweza pia kumfuatilia mwandishi kupitia mitandao ya kijamii:

Facebook: James Kalekwa

Instagram: james_kalekwa

Twitter: @MchungajiJK

Iwapo una ushuhuda, unahitaji ushauri na msaada wa kichungaji unaweza kuwasiliana naye moja kwa moja kupitia +255-754-917-7764 (Kupiga simu, SMS na WhatsApp)

NEW VINE CHURCH Dodoma

# Abudu Nasi

**KILA JUMAPILI - saa 3.00 asbh -6.30 mch**

**KILA ALHAMISI - saa 11.00 jioni -12:15 jioni**



nvc_dodoma +255 754 917 764

Mahali tulipo: **Swaswa - Njia Panda ya Waziri Mkuu**

*A Home of Impact*

# KUHUSU MWANDISHI



James Kalekwa ni amemwamini Yesu kuwa Bwana na Mwokozi wa Maisha yake; ni mtoto wa kiroho wa Mchungaji Goodluck na Ziada Kyara; ni mume mpenzi wa Frida; Baba anayewajibika kwa Joshua-Vision, Charis "Tai", Victor na Priscilla. Ni mchungaji wa New Vine Church - Dodoma.


James Kalekwa

james_kalekwa

@MchungajiJK

+255 754 917 764